**UJUMBE WA DKT. AGNES L. KIJAZI MKURUGENZI MKUU MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA NA MWAKILISHI WA KUDUMU WA TANZANIA KATIKA SHIRIKA LA HALI YA HEWA DUNIANI (WMO) KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA HALI YA HEWA DUNIANI TAREHE 23 MACHI, 2018**

Kila mwaka ifikapo tarehe 23 Machi Tanzania huungana na nchi nyingine wanachama wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (World Meterological Organization - WMO) katika kuadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani (WMD). Kwa kawaida, maadhimisho ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani huambatana na kaulimbiu ambayo inalenga kuongeza uelewa wa umuhimu wa huduma za hali ya hewa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Ni dhahiri kwamba maendeleo katika sekta mbali mbali za kiuchumi pamoja na mambo mengine yanahitaji huduma bora za hali ya hewa zitakazowezesha kupunguza athari zitokanazo na hali mbaya ya hewa.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni **'Jiweke tayari na zingatia taarifa za hali ya hewa'**. Kaulimbiu hii inaelezea umuhimu wa huduma za hali ya hewa kwa sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo na usalama wa chakula, uvuvi na mifugo, afya, nishati, rasilimali maji na uchukuzi. Aidha, kaulimbiu hii inatilia mkazo wa uhitaji wa huduma za hali ya hewa katika kusaidia utekelezaji wa agenda ya kimataifa ya maendeleo endelevu, kupunguza athari za maafa na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama nchi nyingine Duniani hivi karibuni imekumbwa na matukio ya hali mbaya ya hewa kama vile mvua kubwa, ukame na joto kali, ambayo yamesababisha uharibifu wa miundombinu, upotevu wa maisha na mali. Katika kuhakikisha matukio haya yanafuatiliwa, kuwekwa katika kumbukumbu na kuhabarishana miongoni mwa wadau na wafanya maamuzi nchini, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Prof. Makame M. Mbarawa (MB) katika mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania lililofanyika Makao Makuu Dodoma tarehe 7 Machi, 2018 alizindua *Jarida la Klimatolojia la Kila mwaka. Jarida* hili ni nyenzo ya ufuatiliaji na uwekaji kumbukumbu za matukio yasiyo ya kawaida ya hali ya hewa na mabadiliko ya mifumo ya hali ya hewa kwa mwaka husika. Aidha, *Jarida* hili linaongeza uelewa wa mabadiliko ya tabianchi miongoni mwa wadau na jamii ili kuweza kufanya maamuzi sahihi. Pia, katika *Jarida*

hilo, uchambuzi wa matukio ya hali mbaya ya hewa katika mwaka husika kwa maeneo mbalimbali nchini huchapishwa. Taarifa iliyomo katika jarida hilo, ambalo litakuwa linatolewa kila mwaka, itachangia jamii hapa nchini **kujiweka tayari na kuzingatia taarifa za hali ya hewa.**

Aidha, katika kukabiliana na athari za matukio ya hali mbaya ya hewa, Tanzania inaendelea kuongeza uwezo ili **kujiweka tayari na kuzingatia taarifa za hali ya hewa** kupitia njia mbalimbali. Juhudi zilizopo zinalenga katika kuimarisha mfumo wa utaoaji tahadhari kwa kuwashirikisha wadau nchini. Kupitia juhudi hizi, ushirikiano unaongezwa baina ya watoa huduma na watumiaji wa huduma za hali ya hewa ili kuhakikisha kuwa huduma za hali ya hewa ambazo ni mahususi kwa matumizi katika sekta mbali mbali zinatolewa kwa wakati na katika viwango bora. Juhudi hizi pia zinalenga kuliwezesha Taifa **kujiweka tayari na kuzingatia taarifa za hali ya hewa** katika ajenda ya Kitaifa ya kufikia *Uchumi wa Kati wa Maendeleo ya Viwanda, ifikapo 2025.*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ikiwa ni Taasisi yenye dhamana ya utoaji wa huduma za hali ya hewa hapa nchini inaendelea kujijengea uwezo wa kutoa huduma za uhakika. Huduma hizo ni pamoja na utabiri wa kila siku, siku tano, siku kumi, mwezi na msimu unaotolewa kwaajili ya matumizi katika sekta mbali mbali za kiuchumi na kijamii. Katika kufanikisha hilo Mamlaka imeanzisha mfumo maalumu utakaowezesha kufuatilia mabadiliko katika mifumo ya hali ya hewa inayotumika kutoa utabiri na pia kupima uwezo wa Mamlaka katika kutoa utabiri wa maeneo madogo madogo hasa katika ngazi ya wilaya. Katika kutekeleza hili Mamlaka imeanza kutoa utabiri katika ngazi ya wilaya kwa wilaya chache za majaribio zilizoko katika mkoa wa Arusha. Lengo ni kutoa utabiri katika ngazi ya wilaya kwa nchi nzima baada ya zoezi hilo kufanikiwa katika wilaya hizo za majaribio. Viwango vya usahihi wa utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania vimeendelea kuimarika kwa kiasi kikubwa ambapo kwa sasa usahihi wa utabiri ni zaidi ya asilimia themanini (80%) na kiwango hicho ni juu ya kiwango cha chini cha asilimia 70% kinachokubalika kimataifa.

Mafanikio haya yamechochewa na jitihada za Mamlaka kwa kuwezeshwa na Serikali katika kuboresha miundombinu ya hali ya hewa, weledi kwa wataalam na taratibu za kiutendaji. Taratibu hizo za kiutendaji ni pamoja na kufanya kazi kwa kuzingatia viwango vipya vya ubora wa huduma vya

kimataifa (ISO 9001:2015) kama vilivyoanishwa na Shirika la Kimataifa la Viwango Duniani. Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu Barani Afrika mpaka sasa zilizofanikiwa kupata cheti cha Ubora wa utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa usafiri wa anga katika viwango hivyo vipya ambapo viwango vya zamani vimewekewa ukomo wa matumizi mwezi Septemba, 2018. Uboreshaji wa miundombinu unahusisha kuongeza mtandao wa rada za hali ya hewa na vituo vinavyojiendesha vyenyewe, ambapo kwa upande wa weledi, wataalam wamepata mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

Aidha, Mamlaka inakusudia kuijengea jamii uwezo wa kuhimili athari zitokanazo na matukio ya hali mbaya ya hewa kwa kuwashirikisha wadau katika kuandaa tahadhari za hali ya hewa zinazozingatia uratibu wa maafa na kuongeza uelewa kwa jamii na mtu mmoja mmoja. Matumizi sahihi ya tahadhari hizi yatasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza athari zitokanazo na hali mbaya ya hewa. Mamlaka pia inaendelea kuimarisha mfumo wa mawasiliano na usambazaji wa taarifa za hali ya hewa ili kuhakikisha kuwa tahadhari zinaeleweka na zinaifikia jamii iliyoko katika mazingira hatarishi ili kulinda maisha na mali. Katika kufanikisha azma hiyo, Mamlaka inafanya kazi na wadau mbalimbali likiwemo Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) ili kuboresha ufungashaji wa taarifa za hali ya hewa katika lugha nyepesi na inayaoeleweka hivyo kuongeza wigo wa matumizi kwa watoa maamuzi na watumiaji wa taarifa hizo.

Tunapoadhimisha Siku ya Hali ya Hewa duniani mwaka huu wa 2018, Mamlaka inatoa wito kwa jamii na wadau mbalimbali kuendelea kufuatilia na kutumia taarifa za hali ya hewa na ushauri unaotolewa ili kufanikisha malengo yanayokusudiwa. Ni kwa njia hii, tunaweza kutoa mchango wa kuisaidia jamii kujenga uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi na tutakuwa tumetoa mchango kikamilifu kwenye Dira ya nchi ya Maendeleo kufikia 2025 tukizingatia kuwa taarifa za hali ya hewa zina mchango mkubwa katika maendeleo ya viwanda.

Mwisho, nawatakia wadau wote wa hali ya hewa mliopo hapa nchini, muwe na maadhimisho mema ya Siku ya Hali ya Hewa Duniani. Aidha, ofisi mbalimbali za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania zitakuwa wazi, tunawakaribisha mtutembelee na kuendelea kubadilishana uzoefu ili kama nchi **"Tujiweke tayari na kuzingatia taarifa za hali ya hewa".**